BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

<u>BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI</u>

<u>MKUTANO WA KUMI NA TATU</u>

<u>Kikao cha Kwanza – Tarehe 29 Novemba, 2023.</u>
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. KIAPO CHA UAMINIFU CHA MHESHIMIWA MJUMBE WA BARAZA:

**Mhe. Dkt. Mohammed Ali Suleiman**

II. TAARIFA YA SPIKA:

III. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

<u>Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi</u>:

Nakala zote za Gazeti Rasmi la Serikali pamoja na vijalizo vyake kuanzia tarehe 05 Oktoba, 2023.

<u>Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:</u>

Hotuba ya Uwasilishaji wa Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Kuanzisha Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Nam. 11 ya 2003 na Kutunga Sheria ya Ukaguzi wa Umma na Kuweka Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa Kuhusu Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Kuanzisha Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Nam. 11 ya 2003 na Kutunga Sheria ya Ukaguzi wa Umma na Kuweka Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

## IV. MASWALI:

**Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

9. MHESHIMIWA ZAWADI AMOUR NASSOR (Jimbo la Konde): Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

   Tunaipongeza Serikali kwa kuwasaidia wananchi hasa wa kaya masikini kupitia TASAF ikiwa ni pamoja na kaya zetu maskini zilizomo katika jimbo la Konde.

   (a) Kwa kuwa kumekuwa na malalamiko mengi kwa jamii katika uorodheshwaji wa kukidhi kuwa mnufaika wa kaya maskini, je, ni vigezo na utaratibu upi unaotumika katika kuzichambua na kuzipata kaya maskini.

   (b) Kwa kuwa katika jimbo la Konde zipo kaya zenye hali ngumu kabisa na bado hazijaorodheshwa na kuingia kwenye mpango huu. Je, Wizara yako iko tayari kupokea orodha hiyo ya wanakaya walio na hali ngumu kabisa na hawamo katika mpango huu waliomo katika jimbo la Konde.

**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

71. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

    Utafiti umebainisha kwamba asilimia 15% ya wanawake walioolewa wana wake wenza.

    Je, ni kwa kiasi gani elimu ya maadili ya ndoa inayotolewa na kuratibiwa na Afisi ya Mufti Zanzibar imefanikiwa kupunguza idadi ya talaka na migogoro ya wanandoa.

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

23. MHESHIMIWA AZA JANUAR JOSEPH (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

    Katika kuendeleza harakati za kukuza uchumi nchini, Serikali imeamua kujenga masoko katika maeneo tofauti kwa gharama kubwa. Kati ya masoko hayo ni lile soko liliopo Makufuli, shehia ya Welezo.

    (a) Je, Mhe. Waziri unafahamu kuwa soko la Makufuli hadi muda huu haliko katika hali nzuri ya kibiashara.

    (b) Je, ni sababu zipi zinazokwamisha kuimarika kwa biashara katika soko hilo.

    (c) Je, ni lini Serikali itachukuwa hatua madhubuti ya kuliimarisha soko hilo na kuwaondolea hasara kubwa wanayoendelea kuipata wafanyabishara wetu wadogo wadogo waliopo katika soko hilo.

**Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**

24. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

    Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya kuwekeza katika eneo la kimkakati la viwanda liliopo Chamanangwe Pemba.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

2. MHESHIMIWA ABDALLA ABASI WADI (Jimbo la Nungwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

    Mpira wa miguu ni mchezo nambari moja kwa kupendwa hapa duniani. Katika miaka ya 1980 – 1990, mchezo huu ulishika kasi hapa Zanzibar na timu za Zanzibar kwa wakati huo zilifikia kiwango bora kuliko hata timu za Tanzania bara, Kenya na Uganda.

    (a) Je, kuna sababu gani zilizopelekea timu zetu zisishiriki timu za Muungano.

    (b) Je, kuna sababu gani kila mwaka timu zetu zinazidi

kurudi chini hasa kwa michezo ya kimataifa.

**Wizara ya Afya:**

5. MHESHIMIWA ZAWADI AMOUR NASSOR (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Ili kupunguza vifo vya akina mama na watoto lazima Wizara ihakikishe inatoa huduma zilizobora kwa hospitali na vituo vyetu vya afya.

(a) Je, Wizara imejipanga vipi katika kuhakikisha kunapatikana vipimo vikiwemo vya kupimia damu, mkojo na ‘ultrasound’ sambamba na upatikanaji wa dawa za kuongeza damu hasa katika (antenatal care) kipindi cha ujauzito.

(b) Je, Wizara imejipanga vipi katika kuweka wataalamu vituoni (antenatal clinic) na kujua dalili hatarishi za mama mjamzito ili kuepusha matatizo wakati wa ujauzito na kujifungua.

(c) Bado kuna mapungufu katika kuwahudumia mama wajawazito hasa wakati wa kujifungua sambamba na kufanyiwa upasuaji (operation). Je, ni kina mama wangapi waliofariki wakati na baada ya upasuaji kwa mwaka 2021 – 2023 pamoja na watoto wachanga.

30. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Takwimu zinaonesha kwamba katika kila watu wanane, mmoja wao ana tatizo la ugonjwa wa wasiwasi uliopitiliza na wanawake ndio wanaongoza zaidi katika ugonjwa huo.

(a) Je, ni ipi mikakati ya kitabibu ya kuondokana na tatizo hili.

(b) Je, ni zipi athari za kijamii na kiuchumi kutokana na kuongezeka kwa tatizo hili.

(c) Ni zipi dalili za tatizo hili.

82. MHESHIMIWA MWANAJUMA KASSIM MAKAME (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Tunaipongeza Serikali kwa maamuzi yake ya kujenga hospitali za kisasa katika Mikoa na Wilaya zote za Unguja na Pemba.

(a) Je, Serikali imeshazipatia hospitali hizo wafanyakazi wenye sifa kwa kada zote na vifaa vya kisasa na vya kutosha ili kuyafikia malengo ya Mheshimiwa Rais ya kuanzishwa kwa hospitali hizo.

(b) Ni changamoto gani zilizopo kwa sasa kwa zile hospitali ambazo tayari zimeshaanza kutoa huduma.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

16. MHESHIMIWA ZAWADI AMOUR NASSOR (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Kwa kuwa kumekuwa na malalamiko ya wananchi wetu kufikwa na maradhi mengi kutokana na vyakula wanavyokula kulimwa kwa kutumia kemikali.

(a) Je, kwa kiasi gani Wizara yako inayakubali malalamiko hayo.

(b) Je, Wizara ina mkakati gani wa kurejesha kilimo cha asili bila ya matumizi makubwa ya kemikali.

(c) Je, Wizara imefanya utafiti wa kuepuka kutumia kemikali katika kilimo sambamba na wakulima kulima na kupata faida kwa kulima kilimo chenye tija.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

37. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Ni mashirika gani ya ndege ndani na nje ya nchi yamekuwa yakitumika kama fursa nzuri ya kutangaza vivutio vyetu vya utalii Zanzibar na kwa namna gani fursa hizi zinaleta matokeo chanya.

88. MHESHIMIWA ABDALLA ABASI WADI (Jimbo la Nungwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Mavazi ni moja ya viashiria vya kulinda utamaduni wetu ambao kwa muda mrefu umetujengea heshima na kutufanya tufahamike duniani. Hata hivyo, heshima hiyo imeanza kupotea kutokana na watalii wanaofika nchini mwetu hasa sehemu za vijijini kutembea watupu ama nusu uchi, kinyume na utamaduni wetu.

Je, ni hatua gani ambazo Wizara yako imezichukua ili kudhibiti wimbi la watalii wanaotembea vijijini bila ya kuwa na vazi la heshima.

<u>Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:</u>

26. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

(a) Tathmini iko vipi katika suala zima la uwekezaji wa viwanda kwa sasa, ikiwemo viwanda vikubwa vya kati na vidogo vidogo.

(b) Je, ni asilimia ngapi za ajira zinatokana na uwekezaji katika viwanda vyetu.

(c) Je, ni upi mwelekeo na matarajio ya ajira kupitia uwekezaji wa viwanda hivi.

## V. <u>HOJA ZA SERIKALI:</u>

<u>Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:</u>

Hotuba ya Uwasilishaji wa Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Kuanzisha Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Nam. 11 ya 2003 na Kutunga Sheria ya Ukaguzi wa Umma na Kuweka Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo – Kusomwa kwa mara ya Pili.

Zanzibar,
29 Novemba, 2023.

Raya Issa Msellem
<u>KATIBU WA BARAZA</u>.